JAMHURIYA MUUNGANOWA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO 2025

## SHULE YA SEKONDARI MAN'GOTO.

**Kumb Na: MNT/JI/VOL 01/ 2026/01**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P …………………………………..**
**…………………………………………….**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MANG'OTO HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2026/2027.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2026/2027 na atasoma tahasusi ya ........... Kulingana na chaguo lake.

**2.** Shule yetu ina tahasusi (Combinations 3**) HKL, HGK na HGL.** Shule ipo wilaya ya Makete Mkoa wa Njombe, KM 50 kutoka Makete mjini na KM 58 kutoka Njombe standi kuu ya mabasi. Usafiri wa mabasi upo kila siku kuanzia Njombe standi kuu ya mabasi hadi Mang'oto kwa Tsh 6,000 na muda ni saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni kwa mabasi kampuni ya mbalimbali. Shuka Stendi kwenye kibao cha shule ya Sekondari Mang'oto. Usafiri kutoka Makete mjini kupitia Ikonda kuja Mang'oto nao ni wa uhakika, Panda Mabasi yanayoenda Njombe, Shuka Stendi, kwenye kibao cha shule ya Sekondari Mang'oto nauli pia ni Tshs 6,000.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 05/07/2026, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 04/07/2026 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/07/2026.

**3.Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**3.1 Sare za Shule**

**SARE ZA SHULE (WASICHANA**)

1. Suruali 01 (kijani jeshi) na Sketi moja rinda box rangi ya kijani jeshi inayo gusa visigino (Angalia kiambatanisho cha sare za shule hapo chini)-kitambaa kiwe isitimu nzito.
2. kigauni cheupe mshono wa solo fupi na kisivuke magoti kitambaa(polista) kimoja (01) na shati jeupe tomato mikono mirefu 01.
3. Sweta 02 ( kijani jeshi) , gumboot nyeusi jozi moja.
4. Jezi za michezo rangi nyekundu na raba za michezo jozi moja. Michezo ni ya lazima.
5. Viatu vya ngozi jozi mbili rangi nyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu (isiwe aina ya buti).
6. Soksi jozi mbili au zaidi ndefu nyeupe.
7. Track suit moja ya blue (KITAMBAA CHA MTELEZO NA ISIWE NA KOFIA) ADIDAS itavaliwa wakati wa usiku (night preparation).

8. Jacket moja zito jeusi lisilo na kofia na maandishi yoyote kwa ajili ya baridi, majaketi marefu yanayovuka magoti hayaruhusiwi kabisa. (prova haziruhusiwi)
9. Pull neck nyeupe (kabashingo).
10. Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na hijabu nyeupe kwa ajili ya kuvaa darasani wakati wa vipindi na dark blue hizo zitavaliwa na shamba dress.
11. Shamba dress dark blue inayovuka magoti.
12. T-shirt rangi ya blue yenye upinde mweupe shingoni na mikononi (coton) T - shirt hiyo yenye nembo ya shule kwa gharama ya Tsh. 15,000/= inapatikana karibu na shule.

NB

UNASHAURIWA KUWEKA ALAMA VIFAA VYAKO VYOTE MUHIMU HASA SARE ZA SHULE ILI UWEZE KUVITAMBUA KWA URAHISI

**3.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -**

**VIFAA VYA BWENINI**

a) Godoro la sponchi size ft $2\frac{1}{2}$ aje nalo.
b) Mashuka (2) rangi ya pinki, blanketi zito (kuna baridi) kanga au kitenge doti moja,kanda mbili na taulo.
c) Vyombo vya kulia chakula bakuri (hot pot) lenye mfuniko, kijiko na kikombe.
d) Toilet paper, mafuta ya kupaka ya kawaida( vipodozi na pafyumes haziruhusiwi), dawa ya meno, miswaki, kiwi na sabuni.
e) Ndoo mbili za lita 10 zenye mifuniko.
f) Nguo za ndani na Taulo za kike za kutosha.
g) Sanduku (Tranka) la kuhifadhia vifaa 1 na kufuli imara
h) VIFAA VYA USAFI: mwanafunzi aje na vifaa kwa ajili ya usafi wa mazingira ya shule kulingana na tahasusi yake kama ifuatavyo;

| **HKL** | **HGK** | **HGL** |
|---|---|---|
| JEMBE LENYE MPINI 01,HARD BLOOM 01, SOFT BLOOM 01, KWANJA 01, MOPPER 01, SABUNI YA MAJI LITA 5 DEX AU TARMOL. | JEMBE LENYE MPINI 01, SOFT BLOOM 01 ,HARD BLOOM 01, KWANJA 01, MOPPER 01,SABUNI YA MAJI LITA 5 DEX AU TARMOL. | JEMBE LENYE MPINI 01, HARD BROOM 01, SOFT BLOOM01,KWANJA 01, MOPPER 01, SABUNI YA MAJI LITA 5 DEX AU TARMOL. |

**2.1 Michango ya shule**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**FEDHA HIZI ZOTE ZILIPWE BENKI (NMB 6046600006 MKUU WA SHULE MANG'OTO SEKONDARI )**

Andika jina la mwanafunzi unayemlipia na orodhesha vitu vilivyolipiwa. Hatutapokea fedha. Njoo na BPS (BANK PAY SLIP OR HATI YA MALIPO YA BENKI) hapa shuleni na utakatiwa risiti.

**NB: BIMA YA AFYA NI LAZIMA, KILA MWANAFUNZI AJE NAYO.**

## 2.2 VIFAA VYA KITAALUMA

I) Daftari counter books 10 kwa ajili ya notes za masomo yake, school bag ni lazima kwa ajili ya kuhifadhia madaftari hayo.

II) Advanced Dictionary kwa wote

III) Wanaochukua Tahasusi yenye Kiswahili waje na kamusi na wanaochukua Tahasusi yenye Geography waje na Atlas.

IV) Ream A4 (Bunda (02)kwa mwaka. Ream ziwe aina ya a1one kama inavyoonekana kwenye picha hapo. Ream tofauti na hizo hazitapokelewa.




V) Mathematical set (mkebe) kwa wanaosoma Jiografia.

VI) SCIENTIFIC CALCULATOR (ORIGINAL) kwa wanaosoma Geography.

VII) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika ( orodha imeambatanishwa)

**ENGLISH LANGUAGE**

a) James J (2012, Advanced English Language, form six and form five, Oxford university press.

b) Asheri N. (2010) Advanced level English Second Edition, Good book publisher, Dar-es-salaam. Advanced literature

**NOVELS**

a) A man of the people – Chinua Achebe
b) The Rape of the pearl – Magala Nyajo
c) The Beautiful Ones are Not Yet Born- Ayi Kwei Amah

**PLAYS**

a) An enemy of the people – Henrick Ibsen
b) The bride – Austin Bukenya
c) I will Marry When I want- Ngugi Wa Thiong'o

**POETRY**

a) Selected Poems – Institute of Education
b) The wonderful surgeon and other poems – Charles Mloka. c)

**VITABU VYA KISWAHILI Kiswahili II**

a) JPD Company (2008) Kiswahili II kidato cha 5 & 6 General supplies Ltd Dar es salaam. J.A. Masebo (2011) – b) Nadharia ya fasihi k. 5 na 6 Nyambari nyangwine.

**ZIADA**

a) Kaptura la Max – Kezirahabi
b) Rosa Mistika – Kezirahabi
c) Mirathi ya hatari –
d) Moto wa mianzi
e) Ngoma ya mianzi
f) Ngome ya mianzi

**USHAIRI**

a) Kimbunga – Haji Gora
b) Fungate ya Uhuru – Mapenzi bora – Shaban Robert
c) Chungu tamu – T. Mvungi

**RIWAYA**

**a)** Mfadhili – Hussein Tuwa
**b)** Kufikirika – Shabani Robert
**c)** Usiku utakapokwisha – Mbunda Msokile
**d)** Vuta n'kuvute – Shafi A. Shafi

**TAMTHILIYA**

a) Morani – Emmanuel Mbogo
b) Kivuli kinaishi – Said Mohamed
c) Nguzo mama – Penina Mhando
d) Kwenye ukingo wa thim –

**KISWAHILI I**

**a)** Saluhaya (2010) Nadharia ya lugha STC DSM – Tanzania Masebo J.A (2012)
**b)** Nadharia ya Kiswahili kidato cha 5 na 6 G/S FORM V & VI
**c)** Nyambari Nyangwine (2009) Advance Level General Studies notes Nyambari Nyanga

**GEOGRAPHY**

a) Clarke. J. T. (Ed) (1975) An Advanced Geography of Africa.
b) K.K. Sibugu & I.P. Isengum (1986) Outline of soil Science.
c) Msabila D.T. (2003), Success in Geography climatology
d) The Essential of practical Geography advanced level form 5 & 6. Notes, Qn with answers. (J.W.N and F.K. Salosu Jacob)

**HISTORY I & II**


- **a)** Oxford (2011) Advanced learners. History form 5 and 6. Oxford university press (T) Ltd. Dar-essalaam.
- **b)** Kamili 2 (2015) Advanced level. History part one alive. Kot Dublishers.
- **c)** Walter Rodney, (1976) how Europe underdeveloped Africa. TPH, DSM
- **d)** Perry Davis, (1985) History of the world Houghton Milton Company Washington.
- **e)** Modern world History Second Edition (Ben Wash)
- **f)** World history modern Era (Ellis Esler)
- **g)** Advanced History 1 and 2 by Sarehe Yasin
- **h)** Advanced History 1 and 2 by Shibitali


**MUHIMU: KWA KILA MWANAFUNZI HAKIKISHA UNA VITABU VYA MASOMO YA TAHASUSI YAKO KWA AJILI YA KUJISOMEA.**

## 4.Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na :-

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

- i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
- ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
- iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
- v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- ix. Kutunza mali za shule;
- x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
- xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu wala vifaa vinavyohusiana na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya; viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu (mwanafunzi aje na:-)**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali; (imeambatanishwa) ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai (imeambatanishwa)
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; (imeambatanishwa)
iv. Picha nne (4) za passport za mwanafunzi na za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**



**DIONIS VENANCE MGINA**
**MKUU WA SHULE**
**0753026716/0619093130**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MANG'OTO
S.L.P 134 MAKETE NJOMBE

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mzazi wa mtoto husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

➢ **Namba za Simu:**

**Mkuu wa Shule: 0753026716.**

**Makamu mkuu wa shule: 0744677051 / 0626174454**

**Mhasibu wa shule: 0629818838**

**Mwandamizi malezi: 0611203473**

**Mwandamizi Taaluma: 0769966206**

## OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

## SHULE YA SEKONDARI MANG'OTO

### FOMU YA MAPATANO/KUKUBALI NAFASI YA MASOMO NA KUSOMA KATIKA SHULE HII KIDATO CHA ........ MWAKA 2026.

NB: Kabla ya kusaini soma kwa makini maagizo yote kama hutaridhika basi usifike kabisa. Tafuta shule yoyote Tanzania. Shule haitasikiliza vizingizio vya aina yoyote. pia kama afya yako si nzuri fanya utaratibu na mzazi wako kupata shule nyingine ukiwa huko huko, shule haitataka usumbufu wowote. Au KAMA unataka masomo ambayo shule hii hayapo wasiliana na wizara ili ubadilishwe huko huko.

________________________________________

__________________________________________________

______________________________________________________

**JINA LA MWANAFUNZI ANWANI:**
**MIMI**

Nimekubali/sikubali kujiunga na Jamuiya ya shule ya sekondari MANG'OTO. Nimesoma maagizo ya shule kwa makini na kuyaelewa. Naahidi kuwa mtiifu na nitazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Kinyume chake hatua kali zitachukuliwa dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Naahidi kusoma kwa bidii sana masomo yangu na kufaulu mitihani itakayotolewa na shule, Mkoa na Taifa.

Sahihi ya mwanafunzi____________________________Tarehe____________________________________

**B. Mzazi/mlezi**

Mimi nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa kwa mtoto wangu nimekubali /sikubali mwanangu achukue nafasi hiyo. Naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia, Naahidi pia kumlipia karo ya shule/fedha za matibabu/na michango mingine mbalimbali iliyoagizwa na shule kwa wakati mwafaka kinyume chake nichukuliwe hatua za kisheria.

Sahihi ya mzazi /mlezi __________________________Tarehe_____________________

NB: Fomu hii itawekwa kwenye faili au jalada lake.

Andika namba ya simu ya mzazi/Mlezi tu __________________kwa ajili ya mawasiliano na shule.

**PRIME MINISTER'S - OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**MANG'OTO SECONDARY SCHOOL.**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

**TO THE MEDICAL OFFICER.**

___________________________

___________________________

___________________________

PART A: Mr/Mrs/Miss______________________________________________________________

Please examine the above named student as to her/his physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories.

1. Hemoglobin: ____________________________________________________________________

2. P.V. bleeding: ____________________________________________________________________

3. Eye sight: ____________________________________________________________________

4. Blood pressure: ____________________________________________________________________

5. Urine for sugar: ____________________________________________________________________

6. Stool for routine examination: ____________________________________________________________________

7. Skin, Diseases: ____________________________________________________________________

8. Asthma: ____________________________________________________________________

9. Leprosy: ____________________________________________________________________

10. Epilepsy: ____________________________________________________________________

11. Any deformity: ____________________________________________________________________

12. Pulmonary tuberculosis: ____________________________________________________________________

13. Neurosis: ____________________________________________________________________

14. Venereal Diseases: ____________________________________________________________________

15. Pregnant test: ______________________________________________ 16. Other serious Diseases:

____________________________________________________________

Thank you

**DIONIS VENANCE MGINA**
**MKUU WA SHULE**
**0753026716/0619093130**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MANG'OTO
S.L.P 134 MAKETE NJOMBE

**(TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)**

1. I have examined the above named student and consider her that she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for full time schooling.

OTHER COMMENTS: ____________________

2. Date __________Name and Signature________________Designation ______________Official Stamp ______________

**MFANO WA SARE ZA SHULE**

**a) SARE ZA DARASANI -RANGI KIJANI JESHI.**







**B. SHAMBA DRESS**



